Wizara ya Afya

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TMDA

Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

# MWONGOZO WA UHAMASISHAJI WA UTOAJI TAARIFA ZA MAUDHI YATOKANAYO NA MATUMIZI YA DAWA AU CHANJO KWA JAMII



## MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

World Health Organization

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

## 1. UTANGULIZI

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Afya yenye jukumu la kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, chanjo, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa za tumbaku. Pamoja na majukumu mengine, TMDA ina wajibu wa kukusanya na kufuatilia taarifa za maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo ili kulinda afya ya jamii

Mwongozo huu rahisi umeandaliwa kwa ajili ya kuwasaidia wahudumu wa afya kuhamasisha jamii umuhimu na namna ya kutoa taarifa za maudhi yatokanayo na dawa au chanjo nchini.

## 2. UTAMBULISHO NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA KUHAMASISHA UTOAJI TAARIFA DHIDI YA MAUDHI YATOKANAYO NA MATUMIZI YA DAWA AU CHANJO

### (a) Utambulisho na salamu

Kabla ya kuanza kutoa elimu, mhudumu wa afya ajitambulishe na kusalimia walengwa kwa ajili ya kutengeneza mazingira rafiki ya uhamasishaji.

### (b) Eleza umuhimu wa elimu unayotoa ya kuripoti maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo

Eleza kuwa, uhamasishaji wa kutolea taarifa maudhi yatokanayo na dawa au chanjo una lengo la kuwaongezea uelewa wahudumu wa afya pamoja na jamii kuhusu shughuli mbalimbali za ufuatiliaji wa maudhi ya dawa na chanjo unavyofanyika nchini.

### (c) Eleza maana ya maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo

Maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo ni hali isiyotarajiwa inayowapata baadhi

ya watu baada ya kutumia dawa au chanjo katika dozi sahihi. Mfano wa maudhi ni kama vile muwasho wa ngozi, homa, maumivu ya kichwa, viungo, misuli, kuvimba/maumivu ya muda mrefu mahali mtu alipochanjwa, kichefuchefu, kutapika na mengineyo.

## (d) Maudhi yatokanayo na dawa au chanjo huweza kusababishwa na yafuatayo: -

| **1 Maudhi yanayosababishwa na kasoro za uchomaji/utumiaji wa dawa/chanjo** | **2 Maudhi yanayosababishwa na wasiwasi/hofu ya mteja** | **3 Maudhi yatakayotokea kwa bahati tu na yasiyo husiana na dawa au chanjo** |
|---|---|---|
| Ni maudhi yanayohusishwa na kasoro wakati wa utumiaji/uchomaji wa chanjo au uhifadhi wa chanjo/dawa usiofaa | Ni maudhi yanayohusishwa na wasiwasi/hofu ya mteja katika kutumia dawa/chanjo. Hususan dawa za sindano (mf. Kuzimia, kutapika, kutoka jasho jingi, n.k.) | Ni maudhi yanayosababishwa na sababu zingine ambazo hazihusiani na chanjo au dawa iliyotumiwa |

Maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo huweza kuwa madogo au makubwa.

Maudhi makubwa ni maudhi yanayoweza

kusababisha, kulazwa hospitalini au kuongezeka kwa muda kwa mgonjwa alielazwa hospitalini, ulemavu/udhaifu, au madhara anayozaliwa nayo mtoto mchanga kama vile ulemavu, kuhatarisha uhai pamoja na kifo.

Eleza kuwa, bila kujalisha ukubwa wa maudhi au kisababishi chake, maudhi yote yanayotokea mara baada ya kutumia dawa au chanjo yanapaswa kutolewa taarifa TMDA.

**(e) Hatua za kuchukua iwapo mtumiaji wa chanjo amepata maudhi**

Eleza kuwa, ikiwa mtumiaji wa dawa au chanjo amepata maudhi anapaswa kufanya yafuatayo: -

i) Kurudi katika kituo cha kutolea huduma za Afya alichopatiwa dawa/chanjo husika, au kituo kingine chochote cha huduma za afya kilicho karibu kwa ajili ya kupatiwa matibabu na kujaziwa fomu

maalum ya TMDA (fomu ya njano) ya kutolea taarifa hizo au,

ii) Kupiga simu TMDA namba 0800110084 (BURE) kwa ajili ya kupata ushauri na msaada wa haraka.

## (f) Faida zinazopatikana kutokana na utoaji taarifa za maudhi ya dawa au chanjo

Mhudumu wa afya awaeleze washiriki umuhimu wa kutoa taarifa za maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo. Utoaji wa taarifa za maudhi ya dawa au chanjo una madhumuni yafuatayo:-

i) Kusaidia mteja kupata huduma stahiki na kwa wakati muafaka,
ii) Kufahamu kwa undani maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo yanayofahamika au yasiyo fahamika ili kulinda afya ya jamii,
iii) Kufuatilia ili kuhakikisha ubora, usalama na ufanisi wa dawa na chanjo

unazingatiwa kuanzia wakati wa usajili, usafirishaji, uhifadhi na wakati wa matumizi,

iv) Kuboresha afya ya jamii na huduma kwa watumiaji wa dawa na chanjo, na

v) Kuiwezesha Wizara ya Afya kupitia TMDA kufanya maamuzi sahihi dhidi ya usalama wa dawa na chanjo husika ili kulinda afya ya jamii.

## 3. UTOAJI WA TAARIFA ZA MAUDHI YATOKANAYO NA MATUMIZI YA DAWA AU CHANJO

### (a) Taarifa zipi za maudhi zitolewe TMDA?

Elezea kuwa,taarifa za maudhi yoyote ya kiafya yatakayojitokeza baada ya kupatiwa dawa au chanjo hata kama hayaoneshi kuwa na uhusiano wa moja kwa moja yanapaswa kutolewa taarifa na kuripotiwa TMDA mara tu baada ya kutokea.




Maudhi haya yanaweza kuwa yasiyotarajiwa (ikiwa ni pamoja na vipimo vya kimaabara visivyo vya kawaida), dalili au ugonjwa unaohusiana au kutohusiana na dawa au chanjo iliyotumika. Mfano wa maudhi hayo ni kama vile homa, kutapika, kupata ganzi, uvimbe au maumivu makali yasiyo ya kawaida mahali ulipochanja na mengineyo.

Mhudumu wa afya asisitize kuwa ni muhimu taarifa zote za maudhi yanayojitokeza baada ya matumizi ya dawa au chanjo kutolewa taarifa TMDA kupitia njia zilizoainishwa katika kijarida hiki.

**(b) Nani anaweza kutoa taarifa za maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa na chanjo?**

Eleza kuwa, taarifa za maudhi yatokanayo na dawa au chanjo zinaweza kuripotiwa na wafuatao:-

i) Mhusika mwenyewe aliyepata maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo,
ii) Mzazi/mlezi, ndugu au mtu yeyote aliye karibu na aliyepata maudhi ya dawa au chanjo,
iii) Mtaalam wa afya (mfano daktari, mfamasia, muuguzi, afisa afya n.k.)

## (c) Njia zipi hutumika kutoa taarifa za maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo nchini?



Taarifa zozote za maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo zinaweza kutolewa kwa njia zifuatazo:-

i) Fomu maalum ya njano inayojazwa na mtaalam wa afya na kutumwa Makao Makuu ya TMDA au ofisi za TMDA za kanda zilizoko mikoa mbalimbali nchini,

ii) Fomu maalum ya rangi ya kijani

inayojazwa na aliyepata maudhi au mzazi/mlezi/ndugu wa aliye karibu. Fomu hupatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya na kisha hurudishwa vituoni baada ya kujazwa,


iii) Kupitia mfumo wa kieletroniki kwa kufuata kiunganishi cha tovuti sqrt.tmda.go.tz

iv) Kwa kupiga simu namba ***152*00#,** chagua namba **2 (Afya)**, kisha **3 (TMDA)**, kisha **1 (Ripoti maudhi)**, chagua namba 3 (Chanjo) kisha endelea kujaza kwa kufuata maelekezo,

v) Kwa Kupitia "application" ya kieletroniki ya **TMDA** ya kutolea taarifa za maudhi ya dawa/chanjo **(TMDA Adverse Reaction Reporting Tool)** inayopatika na kwa kupakua kutoka kwenye "Google Play Store" kwa kutumia simu janja (smart phone) yenye mfumo wa "Android".

iv) Kwa kupiga simu namba 0800110084

## 4. TAARIFA MUHIMU ZA LAZIMA ZA KUJAZA WAKATI WAKUTOA TAARIFA ZA MAUDHI YATOKANAYO NA MATUMIZI YA CHANJO AU DAWA



Eleza kuwa, wanaojaza au kutoa taarifa za maudhi ya dawa wanapaswa kuzingatia yafuatayo:-

a) Mhudumu wa afya anapojaza fomu ya

njano ahakikishe fomu imejazwa kikamilifu na kwa usahihi, hususan taarifa za umri, jinsia, tarehe ya kupata chanjo au kutumia dawa. Taarifa nyingine muhimu za kujaza ni pamoja na aina ya maudhi na muda yalipoanza na kuisha (au eleza iwapo maudhi bado yanaendelea), jina la chanjo au dawa husika, namba ya toleo la dawa au chanjo (pia taarifa za maji ya kuchanganyia chanjo – diluent). Mwisho, ni muhimu kuweka jina na namba ya simu ya mtoa taarifa na jina la kituo cha kutolea huduma za afya.

b) Vilevile, kwa yeyote atakayejaza fomu ya kijani ahakikishe fomu imejazwa kikamilifu hususan taarifa za umri, jinsia za aliyepata maudhi, tarehe ya kuchanjwa au kutumia dawa. Taarifa nyingine muhimu za kujaza ni pamoja na aina ya maudhi na muda yalipoanza na kuisha (au eleza iwapo maudhi bado yanaendelea), jina la chanjo au dawa

husika, jina na namba ya simu ya mtoa taarifa na jina la kituo cha kutolea huduma za afya dawa au chanjo ilipotolewa.



c) Mzazi au mtu yeyote anapotoa taarifa kwa kupiga simu ya bure namba *152*00#, ahakikishe kuwa: -
   i) Anatuma ujumbe mmoja tu,
   ii) Anaandika kikamilifu na kwa usahihi taarifa za

- Umri na jinsia  za aliyepata maudhi,
- Aina ya maudhi yanayoripotiwa,
- Jina la chanjo au dawa na
- Muda maudhi yalipoanza na kuisha (au eleza iwapo maudhi bado yana endelea),
- Jina la kituo cha kutolea huduma za afya kilichotoa chanjo au dawa husika.

Mhudumu wa afya asisitize kuwa taarifa zote za maudhi yatokanayo na dawa au chanjo hutunzwa kwa usiri mkubwa.

**5. KUMBUKA**

Kutoa taarifa za maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo ni jukumu letu sote kwa ajili ya kulinda afya ya mtu mmoja mmoja, familia au jamii kwa ujumla.

**“Kumbuka: Taarifa moja ya maudhi yatokanayo na matumizi ya dawa au chanjo utakayoitoa, itaboresha afya yako na kulinda afya ya jamii”**

**Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia anuani ifuatayo:**


Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),
S.L.P 1253 Dodoma
Au

Ofisi Ndogo ya Makao Makuu, Barabara ya Mandela, Mabibo – External,
S.L.P 77150 Dar es salaam.
Simu+255 22 2450512/2450751/2450979
+255262961989, 2061990
Barua pepe: info@tmda.go.tz
Tovuti: www.tmda.go.tz
Simu bila malipo: 0800110084

0800110084 @tmda_tanzania @tmda tanzania www.tmda.go.tz